

# Maandalizi uendeshaji SGR yashika kasi TRC

Na Francisca Emmanuel

**W**AFANYAKAZI 14 wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) wanatarajia kwenda nchini Korea Kusini kwa ajili ya kupatiwa mafunzo kwa vitendo ya uendeshaji wa treni ya kisasa ya Standard Gauge (SGR) kuanzia Desemba Mosi mwaka huu.

Hatua hiyo ni utekezaji wa mkataba wa mafunzo kwa vitendo uliosainiwa Julai 4, mwaka huu mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan, kati ya TRC na Shirika la Reli la Korea Kusini (KORAIL).

Akizungumza wakati wa hafla ya kuwaaga wafanyakazi hao jana Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kodogosa alisema wanapeleka wafanyakazi wakapatiwa mafunzo kwa vitendo katika uendeshaji wa treni ya kisasa, mafunzo ambayo yatatolewa kwa miezi mitano kuanzia Desemba Mosi, mwaka huu.

“Wafanyakazi 45 watapatiwa mafunzo ya nadharia hapa nchini ili na wenyewe waweze kujengewa uwezo katika uendeshaji wa treni ya kisasa na kuleta tija katika nchi na shirika kwa ujumla,” alisema Kadogosa.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo yatakuwa katika masuala ya uendeshaji, usalama wa reli, biashara, mitambo, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na miundombinu ya reli ikiwemo ujenzi, ishara, mawasiliano na umeme.

Alieleza kuwa Korea Kusini imeendelea katika masuala ya teknolojia ya uendeshaji wa treni ya kisasa hivyo, aliwataka wafanyakazi hao kuhakikisha wanajifunza kwa bidii kuongeza tija katika shirika hilo.



“Mkajifunze kwa bidii ili mfikie malengo tuliyouwatumia lakini pia mtambue kuwa ninyo bado watumishi wa umma hivyo mnatumwakilisha huko nje ya nchi. Tukipata taarifa za utovu wa nidhamu mtachukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu za utumishi wa umma,” alieleza.

Kadogosa alisema mafunzo hayo ni maandalizi ya uendeshaji wa treni ya kisasa ambayo miundombinu yake kwa kipande cha kwanza cha Dar es Salaam hadi Morogoro imekamili kwa zaidi ya asilimia 97.7 na kipande cha pili kutoka Morogoro hadi Makutu-

pura kimekamili kwa zaidi ya asilimia 91.

Aliongeza kuwa shirika limeamua kuwatumia Korail kutoa mafunzo kwa vitendo kwa watendaji wa TRC kwa sababu uendeshaji wa treni ya kisasa nchini humo ni salama kwa asilimia 99.9 na kwamba wana wataalamu walioboea katika nyanja zote za uendeshaji wa treni hiyo ya kisasa.

Alifanua kuwa uendeshaji wa treni ya kisasa utanza rasmi Februari 2023 baada ya taratibu zote za majaribio kufanyika na kubiliana gharama za usafirishaji na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

## Serikali yahadharisha wahitimu IFM

Na Mwandishi Maalumu

**N**AIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Hamadi Hassan Chande amewataka wahitimu wa vyuo mbalimbali nchini hususani Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), kufanya kazi kwa ubunifu, uaminifu na uadilifu na kujiepusha na vitendo vya rushwa, ufisadi, wizi na matumizi ya dawa za kulevya.

Alitoa rai hiyo mkoani Dar es Salaam wakati wa mahafali ya 48 ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) katika Kampasi Kuu ya Dar es Salaam, ambapo zaidi ya wahitimu 4,000 wametunukiwa tuzo mbalimbali

Alisema kuwa IFM imekuwa mstari wa mbele katika kuongeza idadi ya Watanzania wenye taaluma na utaalamu katika sekta ya fedha, uhasibu, bima na hifadhi za jamii hivyo ni vema idadi hiyo iendane na kukidhi mahitaji ya soko ambayo yanahitaji wanataaluma wenye weledi na uadilifu.

Chande alipongeza uongozi wa chuo hicho kwa kuzalisha wataalamu katika fani mbalimbali na kulivezesha taifa kufikia malengo yake ya kujitosheleza katika fani za fedha kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi, kiteknolojia, kisiasa na kijamii.

Kwa upande wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, Chande, alisema serikali itaendelea kuongeza kiwango cha wanafunzi wanaopata mikopo mwaka hadi mwaka ili wenyewe sifa waweze kunufaika.

Katika mahafali hayo, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Dk Imanueli Mnzava, alisema chuo kimeendelea kurahisisha upatikanaji wa mafunzo kwa wananchi kwa kusogeza huduma za mafunzo hayo karibu na wahitaji.

“Chuo kina kampasi Mwanza, Dodoma, Simiyu na sasa tunamalizia ujenzi Kampasi ya Geita kwa ufadhili wa serikali, kama tunavyofahamu elimu ni chachu ya mabadiliko ya kitabia, kiutendaji na uwezo wa kubadilisha mazingira yanayotuzunguka,” alisema Dk Mnzava.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la Chuo, Profesa Emanuel Mjema alisema Baraza la Uongozi la Chuo litaeendelea kusimamia utekezaji wa malengo ya chuo na kuinisha vipaumbele kwa kuzingatia misingi ya tija na upatikanaji rasilimali ili kuboresha viwango vya wahitimu watakaoweza kujijaji, kujitegemea na kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kilianzishwa mwaka 1972 kikiwa na uwezo wa kutoa kozi mbili. Chuo hicho kinatoa zaidi ya kozi 33 katika fani mbalimbali ikiwemo Fedha, Bima, Uhasibu na nyinginezo ambapo hadi mwaka 2021, kulikuwa na wahitimu 39,723. Jana wamehitimu 59.

## Jenista aipa maagizo bodi serikali mtandao

Na Selemani Nzaro

**W**AZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama ameitaka Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao kuzingatia na kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kuwajengea uelewa wadau kuhusu umuhimu wake katika ustawi wa taifa.

Jenista aliyasema hayo hivi karibuni alipozindua Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao mkoani Dar es Salaam. Aliitaka bodi hiyo ifanye kazi kwa uadilifu mkubwa ili kuwa mfano wa kuigwa.

Aliitaka itambue mipaka yake na wajibu wake na itoe ushirikiano kwa menejimenti katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa utekezaji wa shughuli zake kulingana na mpango mkakati.

“Wajumbe wote wa bodi mtashirikiana kikamilifu na wizara kuhakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inatumika katika kuboresha utend-

aji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa umma, zipatikane kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu,” alisema.

Jenista aliongeza kuwa bodi hiyo itapimwa kutokana na ufumbuzi wa changamoto mbalimbali kama upungufu wa wataalamu walioboea katika usanifu, ujenzi na uendeshaji wa mifumo na miundombinu na usalama wa Tehama katika taasisi za umma pamoja na kuongezeka kwa matishio ya usalama wa mtandao na mabadiliko ya haraka ya teknolojia.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Benedict Ndomba, alisema bodi itahakikisha utekezaji wa jitihada za serikali mtandao katika taasisi za umma unaozingatia sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao, Dk Mussa Kissaka alisema atahakikisha utendaji wa bodi hiyo utakuwa wa viwango na wenye msaada kwa serikali ili kukidhi kiu na maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuiona bodi ikiwa msaada mkubwa kwa serikali.

LJ INTERNATIONAL LTD DEBT COLLECTORS/AUCTIONEERS				
TANGAZO LA MNADA WA HADHARA				
Kampuni ya LJ INTERNATIONAL LTD kwa idhini tuliyopewa na benki ya CRDB BANK PLC, tunatoa taarifa ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa wadau/wadhamini wafuatao kulipa madeni yao yote wanayodaiwa na benki hiyo pamoja na gharama za dalali. Iwapo watashindwa kufanya hivyo kwa muda uliyotolewa, tutafanya mnada wa hadhara wa kuzaa dhama zao kama ratiba inavyoonyesha kwenye jedwali hapa chini:				
Na.	JINA	TAWILA BENKI	MAHALI DHAMANA ILIPO	TAREHE YA MNADA
1.	Prisca Alphonse Mapunda	Mbezi Luis	Dhamana iliyopo kwenye kiwanja kisichopimwa eneo la Kwembe Luguruni, Manispaa ya Ubungu.	14/12/2022 kuanzia saa nne asubuhi
2.	Abdallah Said Ngozi	Manyoni	Nyumba iliyopo katika eneo lisilopimwa Songambebe, Wilaya ya Itigi, Manispaa ya Singida	17/12/2022 kuanzia saa nne asubuhi
3.	Mathias Paschal Masanja t/a Exodus Stationery Service Machine	Manyoni	Dhamana ipo Kaloleni, Manispaa ya Singida	14/12/2022 kuanzia saa nne asubuhi
4.	Mathias Paschal Masanja t/a Exodus Stationery Service Machine	Manyoni	Dhamana iliyo katika Kitalu AA, eneo la Mwembeni, Wilaya ya Manyoni	14/12/2022 kuanzia saa nne asubuhi
<b>MASHARTI YA MNADA:</b>				
(a) Mmuni atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa katika mnada siku hiyo ya mnada, na salio la 75% litalipwa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada huo.				
(b) Endapo mmuni atashindwa kulipa salio la 75% kwa muda huo wa siku kumi na nne atakuwa amepoteza haki zake, nyumba itauzwa upya na malipo ya 25% hayatarudishwa.				
(c) Wateja wataruhusiwa kukagua mali husika siku tatu (3) kabla ya mnada.				
(d) Mali itauzwa kama ilivyo.				
(e) Gharama za usajili na ubadilishaji wa umiliki ni jukumu la mmuni.				
Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi: Mkurugenzi Mkuu, LJ International Ltd, Makao Makuu Dar es Salaam, NSSF Building, Tel: +255 22 212 6221, 0743-911921.				